TANGAZO LA SERIKALI NA. 893 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mtendaji wa Kijiji" maana yake ni afisa aliyeajiriwa kama mtendaji wa kijiji na itajumuisha mtaalamu yeyote ndani ya kijiji anayefanya kazi za Afisa Mtendaji wa Kijiji katika kijiji husika;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na mizigo

kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kipindi maalum cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara kwa Halmashauri;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya abiria;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi ikiwa ni pamoja na maeneo ya taasisi ya umma au watu binafsi yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maegesho" sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"mnunuzi wa mazao" maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni, kiwanda au shirika linalonunua mazao kwa ajili ya biashara au matumizi mengineyo katika eneo la Halmashauri;

"muuzaji"maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu,

kampuni, kiwanda au shirika anayeuza au anayesafirisha mazao kutoka Kata moja kwenda kata nyingine au nje ya eneo la Halmashauri mwenye mazao yenye uzito wa zaidi ya tani moja;

"soko" maana yake ni eneo liliotengwa na Halmashauri kutumika kwa shughuri za biashara;

"ada au ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa au unaokusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa madini ya ujenzi" maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa kokoto, mawe, changarawe, mchanga, marumalu, kifusi, udongo mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi, na inajumuisha tozo kwa mtu yeyote atakayesafirisha madini ya ujenzi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine;

"utamaduni" maana yake ni sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi,muziki wa asili,ususi,michezo,muziki wa dansi,video,muziki wa taarabu,maonyesho ya sinema, mazingaombwe,tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

5.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa kwenye kanuni hii.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na mara baada ya malipo mlipaji atapaswa kupewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ushuru wa soko

6.-(1) Kutakuwa na ushuru wa soko utakaolipwa kwa Halmashauriau Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(2) Mtu yeyote atakayefanya biashara kwenye maeneo ya soko ambaye hana kitambulisho cha ujasiriamali kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria hii atapaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa sheria hii.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza bidhaa nje ya eneo la soko au kuanzisha soko bila kibali cha Halmashauri.

(4) Kila soko litakuwa wazi kuanzia saa moja kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili kamili jioni.

Ushuru wa mazao

7.-(1) Kutakuwa na ushuru wa mazao utakaotozwa na Halmashauri kwa-

(a) mnunuzi wa mazao pindi anunuapo mazao kutoka kwa muuzaji katika eneo la Halmashauri;

(b) mtu yeyote atakayesafirisha mazao zaidi ya tani moja kutoka eneo lolote la Halmashauri.

(2) Viwango vya ushuru wa mazao kwa mujibu wa aya hii utakuwa kama ambavyo imeainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii:

(3) Halmashauri haitatoza ushuru wa mazao kwa mtu yeyote ambaye analima kwa ajili ya kujikimu na familia yake mwenye mazao yasiyozidi tani moja.

(4) Mtu yeyote atakayesafirisha mazao yasiyozidi tani moja atatakiwa kuwa na barua kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji wa sehemu aliyolima mazao yake ambayo itathibitisha kwamba mtu huyo amelima shamba katika Kijiji chake.

(5) Katika kupata hesabu ya tani moja yatahesabiwa magunia kumi yenye ujazo usiozidi debe nane kama ndio sawa na tani moja.

Kibali cha kusafirisha mazao

8.-(1) Kutakuwa na kibali cha kusafirisha mazao kitakachotolewa na Halmashauri kwa Mnunuzi wa mazao atakayesafirisha mazao yake nje ya eneo la Halmashauri kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria hii.

(2) Kibali cha kusafirisha mazao hakitawahusu wafanyabiashara wanaosafirisha mazao ya chakula cha mifugo kama vile pumba laini, mashudu na mazao mengine yanayoendana na hayo.

(3) Kibali kilichotajwa katika aya ndogo ya (2) kitapaswa kulipiwa kiasi cha Shilingi elfu ishirini.

Ushuru wa huduma

9.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na ushuru wa bidhaa kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii kutoka kwa wafanyabiashara wenye leseni za biashara ambao hawawasilishi hesabu za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye anawajibika kulipa ushuru wa huduma kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa za hesabu za mwaka kwa ajili ya kukokotoa kiwango.

(4) Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma kwa walipa ushuru wa huduma wanaowasilisha taarifa za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na walipa ushuru wa huduma katika kipindi maalum cha hesabu.

(5) Kila mlipa ushuru wa huduma atatakiwa kulipa ushuru wa huduma si zaidi ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi.

Uteuzi wa wakala

10.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kamati ya Mapato

12.-(1) Kutakuwa na Kamati yakufatilia mapato ya Halmashauri itakayoundwa na Mkurugenzi ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuratibu utendaji kazi wa kikosi kazi cha kukusanya mapato;
(b) kuishauri Halmashauri kuhusu namna ya kuongeza mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato;
(c) kufanya tathmini ya makusanyo katika kila chanzo kwa mwaka ili kuweka maoteo ya mwaka unaofuata.

(2) Kamati ya mapato itawajibika kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa Menejimenti kila mwezi kuonesha namna ilivyofanya kazi katika kipindi husika.

Kikosi kazi cha kudhibiti mapato

13.-(1) Kutakuwa na kikosi kazi cha kufuatilia na kudhibiti mapato ambacho kitaundwa na Mkurugenzi kikihusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali za Halmashauri.

(2) Kikosi kazi kitakachoundwa kwa mujibu wa Sheria hii kitawajibika kwa Kamati ya Mapato.

Makosa

14. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa au atadharau au atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;
(e) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; na
(f) atatumia chombo chochote kile kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

15. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na.

17. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya Mwaka 2019 na

693 la 2019 na 364 la 2013

Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya Mwaka 2013 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya 4(1, )6(2), 7(2) na 9(2))*

SEHEMU YA KWANZA: ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

| Namba. | Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ukaguzi wa nyama ya Ng'ombe baada ya kuchinjwa | 3,000/= kwa kila ng'ombe |
| 2. | Ukaguzi wa nyama ya Mbuzi na Kondoo baada ya kuchinjwa | 1,000/= kwa kila mbuzi au kondoo |
| 3. | Ukaguzi wa nyama ya Nguruwe baada ya kuchinjwa | 1,500/= kwa kila nguruwe |

SEHEMU YA PILI: ADA YA UWAMBAJI NGOZI

| Namba. | Mnyama | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 500/= kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi au Kondoo | 500/= kwa kila mmoja |

SEHEMU YA TATU: ADA YA KUPIMA AFYA

| Namba. | Huduma | Kiwango cha Ada(Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kupima Afya kwa mtu mmoja | 5,000/= kila baada ya miezi sita |

SEHEMU YA NNE:
A: USHURU WA MAZAO YA MISITU (TIMBAO)

| Namba. | Aina ya zao | Kipimo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkaa | kwa gunia la kilo 50 | 3% ya TFS +1,000 |
| 2. | Mbao | kwa ubao (zisizoainishwa ujazo) | 200/= |
| 3. | Mbao | kwa ubao (zisizoainishwa ujazo) | 3% ya TFS + 1,000 |
| 4. | Kuni | kwa mita za ujazo | 3% ya TFS +500 |
| 5. | Fito | kwa mita za ujazo | 3% YA TFS + 200 |
| 6. | Boriti | kwa Boriti (zisizoainishwa ujazo) | 2,000/= |
| 7. | Boriti | kwa mita za ujazo | 3% TFS +500 |
| 8. | Mianzi | kwa mwanzi | 100/= |

B: USHURU WA MAZAO YA MISITU (YASIYO TIMBAO)

| Namba. | Aina ya zao | Kipimo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Uyoga | kwa kilogramu | 500/= |
| 2. | Ukindo | kwa kilogramu | 500/= |
| 3. | Kamba | kwa kilogramu | 500/= |
| 4. | Asali | kwa kilogramu | 500/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Nta | kwa kilogramu | 500/= |
| 6. | Dawa za mizizi | kwa kilogramu | 3,000/= |
| 7. | Dawa za majani | kwa kilogramu | 3,000/= |

C: ADA YA USAJILI WA BIASHARA YA MALIASILI, UVUVI NA MAZINGIRA

| Namba. | Biashara | Kipimo | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Karakana ya uvunaji mkaa, mbao na kuni | Usajili kwa mwaka | 20% ya tozo ya Serikali Kuu |
| 2. | Biashara ya bucha ya wanyamapori | Usajili kwa mwaka | 20% ya tozo ya Serikali Kuu |
| 3. | Tathimini ya athari ya mazingira | Kibali kwa tathimini | 20,000/= kwa kila kazi |
| 4. | Shughuli za uwindaji | Kibali kwa mwaka | 20% ya tozo ya Serikali Kuu |
| 5. | Ada ya usajili wa maduka yanayouza samaki, dagaa wabichi. | Usajili kwa mwaka | 25,000/= |
| 6. | Ada ya leseni ya kuendesha biashara ya samaki, dagaa wakavu. | Usajili kwa mwaka | 25,000/= |

SEHEMU YA TANO: ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTALII KWENYE MAENEO YANAYOSIMAMIWA NA HALMASHAURI

| Namba. | Aina ya shughuli | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Uhudumiaji wa utalii (tour operator) | 50,000/= kwa mwaka |
| 2. | Biashara ya vivutio kwa watalii (curio shops entertainment) | 50,000/= kwa mwaka. |
| 3. | Kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii;mtalii kutoka ndani ya nchi | 500/= kila anapoingia |
| 4. | Kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii;mtalii kutoka nje ya nchi | 1,000/= kila anapoingia. |
| 5. | Kuweka kambi (tented or camping site) | 50,000/= kwa mwaka kwa eneo. |
| 6. | Shughuli nyingine yoyote yenye sura ya utalii | 1,000/= kwa kila mtu |

*Tangazo La Serikali Na. 893 (Linaendelea)*

SEHEMU YA SITA: USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba. | Aina ya Madini | Kiasi (Shilingi) | Ujazo |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchanga, Changarawe, Kokoto, Mawe na Kifusi | 7,000/= | kwa kila gari lenye uzito wa tani 7 inayochimbwa au kusafirishwa |
| | | 5,000/= | kwa gari lenye uzito wa chini ya tani 7 |
| | | 3,000/= | kwa powertiller |
| 2. | Kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kwenye eneo la mtu binafsi kwa mmiliki wa eneo | 500,000/= | kwa mwaka |
| 3. | Kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kwenye eneo la Kampuni | 1,000,000/= | kwa mwaka |

SEHEMU YA SABA: KODI YA PANGO, MAJENGO NA VIBANDA VYA HALMASHAURI

(Viwango hivi vitabadilika kwa kuhuishwa kwenye mikataba ya upangaji iwapo itahitajika kufanya hivyo)

| Namba. | Aina ya jengo | Kodi ya pango inayopendekezwa | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Vibanda ndani na nje ya soko | 30,000/= | kwa mwezi |
| 2. | Vibanda ndani nan je ya stendi | 50,000/= | kwa mwezi |
| 3. | Nyumba ndogo za Halmashauri NHC | 70,000/= | kwa mwezi |
| 4. | Nyumba ndogo za Halmashauri ambazo siyo NHC | 60,000/= | kwa mwezi |
| 5. | Nyumba kubwa za Halmashauri | 100,000/= | kwa mwezi |
| 6. | Kuweka mnara wa mawasiliano kwenye eneo la Halmashauri | 500,000/= | kwa mwezi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Kukodi eneo la Halmashauri kwa ajili ya kuendesha bustani | 200,000/= | kwa mwezi |

SEHEMU YA NANE: ADA YA HUDUMA YA VYOO VYA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya Jengo | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Choo cha Stendi | 300/= kwa kila mtu |
| 2. | Choo cha Soko kuu | 300/= kwa kila mtu |

SEHEMU YA TISA: USHURU WA MAZAO

| Namba | Aina ya Zao | Kiwango cha ushuru (Shilingi) | Kipimo |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 2,000 /= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 100 |
| 2. | Mchele | 2,000/= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 100. |
| 3. | Mpunga | 1,000/= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 75 |
| 4. | Maharage | 2,000/= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 90 |
| 5. | Karanga | 500/= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 90 |
| 6. | Alizeti | 1,000/= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 40. |
| 7. | Muhogo au Udaga au Makopa au uwele au viazi | 500/= | Sawa na 3% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila gunia la kilo 90. |
| 8. | Mazao mengine ya chakula ambayo hayakutajwa | 500/= | Sawa na 2% ya bei ya kununulia ambayo itatozwa kwa kila kilo kwa kiasi kinachozidi tani moja. |
| 9. | Mazao mengine ya | 500/= | Sawa na 2% ya bei ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | biashara ambayo hayakutajwa | | kununulia ambayo itatozwa kwa kila kilo kwa kiasi kinachozidi tani moja. |
| 10. | Vyakula vya mifugo | 500/= | kwa gunia la kilo 100 |

SEHEMU YA KUMI: USHURU WA SOKO NA MAGULIO

| Namba. | Aina ya Bidhaa | Kiasi (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Nguo za mitumba | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 2. | Nafaka rejareja | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 3. | Migahawa ndani ya soko | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 4. | Samaki rejareja | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 5. | Mboga za majani | 500/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 6. | Dagaa rejareja | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 7. | Wauza vyungu | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 8. | Miwa rejareja | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 9. | Matunda, Nyanya, Vitunguu zaidi ya debe mbili | 500/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 10. | Viatu rejereja | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |
| 11. | Bidhaa zote zinazouzwa ndani ya soko kila siku | 500/= | Kila siku |
| 12. | Bidhaa nyinginezo zinazoletwa siku ya gulio ambazo hazikutajwa | 1,000/= | Kwa siku ya gulio tu |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA: USHURU WA MINADA

| Namba. | Aina ya Mnyama | Kiasi (Shilingi.) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | 4,000/= | kwa kila Ng’ombe |
| 2. | Mbuzi au Kondoo | 1,000/= | kwa kila Mbuzi au Kondoo |
| 3. | Nguruwe | 1,000/= | kila Nguruwe |
| 4. | Kuku au Bata | 1,000/= | kwa tenga |
| 5. | Punda | 4,000/= | kila punda |

*Tangazo La Serikali Na. 893 (Linaendelea)*

SEHEMU YA KUMI NA MBILI: USHURU WA STENDI NA MAEGESHO

| Namba. | Aina ya Gari | Kiasi (Shilingi) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Lori au Mabasi au kirikuu litakaloegeshwa stendi | 2,000/= | kwa safari |
| 2. | Hiace na costa | 2,000/= | kwa safari |
| 3. | Teksi | 1,000/= | kwa safari |
| 4. | Bajaji au Pikipiki au Guta | 500/= | kwa safari |
| 5. | Magari ya watu binafsi | 1,000/= | kwa siku |
| 6. | Gharama ya kutunza gari lililokamatwa | 10,000/= | kwa siku |
| 7. | Lori litakaloegeshwa kwenye maegesho ya Halmashauri | 5,000/= | kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA TATU: ADA KWA AJILI YA SHUGHULI ZA UTAMADUNI NA BURUDANI

| Namba. | Shughuli | Kiwango (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Usajili kumbi za muziki na starehe | 200,000/= | kwa mwaka |
| 2. | Matangazo ya burudani ya kutumia vyombo | 30,000/= | kwa kila tangazo kwa siku. |
| 3. | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | 30,000/= | kwa kila tangazo |
| 4. | Fete | 20,000/= | kwa mwezi |
| 5. | Kibali cha kuonyesha sanaa na muziki | 30,000/= | kwa kila onyesho |
| 6. | Kibali cha matamasha | 50,000/= | kwa tamasha |
| 7. | Tozo kwa Baa zinazochezesha muziki | 30,000/= | kwa mwaka |
| 8. | Tozo kwa mchezo wa Pool Table | 20,000/= | kwa mwaka |
| 9. | Tozo kwa kumbi za muziki na starehe | 40,000/= | kwa mwaka |
| 10. | Tozo kwa kumbi za sherehe | 50,000/= | kwa sherehe |
| 11. | Tozo za kurekodi filamu na video | 50,000/= | kwa mwaka |
| 12. | Maonyesho ya mavazi na mashindano ya urembo | 40,000/= | kwa onyesho |
| 13. | Maonyesho ya video | 30,000/= | kwa mwaka |
| 14. | Maonyesho ya mazingaombwe | 10,000/= | kwa siku |
| 15. | Tozo kwa washereheshaji kwenye kumbi za sherehe | 10,000/= | kwa siku |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16. | Tozo kwa mpambaji kwenye kumbi za sherehe | 10,000/= | kwa siku |
| 17. | Tozo kwa Mpishi wa chakula kwenye kumbi za sherehe | 10,000/= | kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA NNE: ADA YA KUZOA TAKA NGUMU

| Namba. | Eneo la usafi | Ada (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Eneo la makazi | 2,000/= | kwa mwezi |
| 2. | Mgahawa | 3,000/= | kwa mwezi |
| 3. | Nyumba za kulala wageni | 5,000/= | kwa mwezi |
| 4. | Taasisi za umma (mashule au hospitali au ofisi za umma kama Tanesco au Posta au Maji)<br>Taasisi za dini na binafsi | 5,000/= | kwa mwezi |
| 5. | Taasisi binafsi kama benki na taasisi za fedha zingine | 20,000/= | kwa mwezi |
| 6. | Supermarket au Mini Market | 10,000/= | kwa mwezi |
| 7. | Karakana za mbao | 5,000/= | kwa mwezi |
| 8. | Wauzaji wa mbao | 2,000/= | kwa mwezi |
| | Wauzaji wa dawa za asili | 5,000/= | kwa mwezi |
| 9. | Karakana za vyuma | 5,000/= | kwa mwezi |
| 10. | Maduka ya jumla | 10,000/= | kwa mwezi |
| 11. | Maduka ya samaki wabichi | 5,000/= | kwa mwezi |
| 12. | Maduka ya rejereja | 5,000/= | kwa mwezi |
| 13. | Baa | 10,000/= | kwa mwezi |
| 14. | Glocery | 5,000/= | kwa mwezi |
| 15. | Kilabu cha pombe | 2,000/= | kwa mwezi |
| 16. | Bucha | 5,000/= | kwa mwezi |
| 17. | Kituo cha mafuta | 10,000/= | kwa mwezi |
| 18. | Gereji | 10,000/= | kwa mwezi |
| 19. | Biashara ya vyuma chakavu | 3,000/= | kwa mwezi |

*Tangazo La Serikali Na. 893 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 20. | Duka la kuoka mikate | 5,000/= | kwa mwezi |
| 21. | Vibanda vya huduma za kifedha kwa njia ya simu | 2,000/= | kwa mwezi |
| 22. | Maduka ya madawa muhimu | 5,000/= | kwa mwezi |
| 23. | Maduka ya madawa ya kilimo na mifugo | 5,000/= | kwa mwezi |
| 24. | Kumbi za starehe | 5,000/= | kwa mwezi |
| 25. | Depot ya bia na soda | 10,000/= | kwa mwezi |
| 26. | Vibanda vya chipsi na nyama | 3,000/= | kwa mwezi |
| 27. | Vibanda vya kuuza mikungu ya ndizi | 5,000/= | kwa mwezi |
| 28. | Wauzaji wa mahindi ya kuchoma | 2,000/= | kwa mwezi |
| 29. | Vibanda au Meza ya biashara ndogondogo | 1,500/= | kwa mwezi |
| 30. | Maduka biashara ya nguo za mitumba | 1,000/= | kwa mwezi |
| 31. | Maduka ya nguo za spesho | 2,000/= | kwa mwezi |
| 32. | Saluni za wanawake | 3,000/= | kwa mwezi |
| 33. | Saluni za wanaume | 3,000/= | kwa mwezi |
| 34. | Studio au video library | 3,000/= | kwa mwezi |
| 35. | Mashine za kukamua mafuta | 5,000/= | kwa mwezi |
| 36. | Mashine za kukoboa mpunga | 10,000/= | kwa mwezi |
| 37. | Mashine za kukoboa na kusaga mahindi | 5,000/= | kwa mwezi |
| 38. | Fundi cherehani | 2,000/= | kwa mwezi |
| 39. | Wauzaji wa viatu vya mtumba | 2,000 | kwa mwezi |
| 40. | Wauzaji wa vitunguu | 2,000/= | kwa mwezi |
| 41. | Vibanda vya kuonesha picha mjongeo au sinema au mpira | 2,000/= | kwa mwezi |
| 42. | Vijiwe vya maroli au powertiller | 3,000/= | kwa mwezi |
| 43. | Vijiwe vya boda boda | 2,000/= | kwa mwezi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 44. | Vibanda vya kuuza matunda | 2,000/= | kwa mwezi |
| 45. | Pool table ambayo haiko kwenye baa | 1,000/= | kwa mwezi |
| 46. | Biashara ya kubahatisha isiyo kwenye baa | 3,000/= | kwa mwezi |
| 47. | Eneo la kuoshea magari | 5,000/= | kwa mwezi |
| 48. | Vibanda ya kutengeneza alluminium | 10,000/= | kwa mwezi |
| 49. | Wauzaji wa miwa nje ya sokoni | 4,000/= | kwa mwezi |
| 50. | Duka la magodoro | 5,000/= | kwa mwezi |
| 51. | Watengenezaji wa vifaa vya umeme | 2,000/= | kwa mwezi |
| 52. | Biashara ya Stationary | 5,000/= | kwa mwezi |
| 53. | Night club | 10,000/= | kwa mwezi |
| 54. | Ofisi za wanasheria au wakandarasi wa umeme | 2,000/= | kwa mwezi |
| 55. | Wauzaji wa samani au sofa | 5,000/= | kwa mwezi |
| 56. | Duka la vifaa vya ujenzi | 10,000/= | kwa mwezi |
| 57. | Biashara ya kujaza upepo | 2,000/= | kwa mwezi |
| 58. | Eneo la ufundi pikipiki | 5,000/= | kwa mwezi |
| 59. | Biashara ya spare za magari au pikipiki au bajaji | 5,000/= | kwa mwezi |
| 60. | Fundi viatu | 1,000/= | kwa mwezi |

SEHEMU YA KUMI NA TANO: ADA YA UKAGUZI WA USAFI WA MAZINGIRA

| Namba. | Maelezo | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Eneo la chakula | 3,000/= kwa mwaka |
| 2. | Nyumba ya kulala wageni | 5,000/= kwa mwaka |
| 3. | Gereji | 3,000/= kwa mwaka |
| 4. | Eneo la kupumzika | 3,000/= kwa mwaka |
| 5. | Hoteli | 10,000/= kwa mwaka |
| 6. | Viwanda | 15,000/= kwa mwaka |
| 7. | Mashine za mpunga | 15,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA SITA: ADA YA UKAGUZI WA RAMANI ZA MAJENGO NA KIBALI CHA UJENZI

| Namba. | Aina ya kibali | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kuweka mnara wa simu | 100/= kwa mita moja ya mraba |
| 2. | Kujenga nyumba ya | 100/= kwa mita moja ya mraba |

| | | |
|---|---|---|
| | makazi | |
| 3. | Kujenga nyumba ya biashara | 100/= kwa mita moja ya mraba |
| 4. | Kujenga shule binafsi na Hospitali binafsi | 100/= kwa mita moja ya mraba |
| 5. | Maghala na bohari | 100/= kwa mita moja ya mraba |
| 6. | Kituo cha mafuta | 200/= kwa mita moja ya mraba |
| 7. | Ghorofa | 200/= kwa mita moja ya mraba |

SEHEMU YA KUMI NA SABA*:* ADA YA MABADILIKO YA JENGO

| Namba. | Aina ya kibali | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya makazi | 50/= kwa kila mita ya mraba |
| 2. | Nyumba ya biashara | 50/= kwa kila mita ya mraba |
| 3. | Ghorofa | 50/= kwa kila mita ya mraba |
| 4. | Majengo mengine | 50/= kwa kila mita ya mraba |

SEHEMU YA KUMI NA NANE: USHURU WA KUEGESHA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA

| Namba. | Aina ya Gari | Kiwango cha Ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari au basi kubwa zaidi ya tani 7 | 2,500/= kwa siku |
| 2. | Magari madogo (Hiace na Noah) | 1,500/= kwa siku |
| 3. | Teksi | 1,000/= kwa siku |
| 4. | Magari binafsi yasiyo ya biashara | 500/= kwa siku |
| 5. | Gari dogo la mizigo (lori au pick up) chini ya tani 7 | 2,000/= kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA TISA: USHURU WA HUDUMA KWA WAFANYABIASHARA WASIOFUNGA HESABU

| Namba. | Ada ya Leseni | Kiwango cha malipo ya ushuru wa huduma (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Leseni kuanzia shilingi 10,000-20,000 | 5,000/= |
| 2. | Leseni kuanzia shilingi 25,000-40,000 | 10,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Leseni kuanzia shilingi 45,000-60,000 | 15,000/= |

JEDWALI LA PILI
(*Limetengenezwa chini ya aya ya 8(1)*)
KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO NJE YA WILAYA
(Transportation Permit for Crop Produce Outside the District)
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

(Permit No.)…………………………………….

Tarehe ya Kutolewa (Date of Issue)……………………………….
Jina la Msafirishaji (Transporter's Name)…………………………
Aina ya Gari (Vehicle Type)………………………………………
Namba ya Gari (Vehicle Registration No.)………………………..

1. Kibali kimetolewa kwa (Permit is hereby granted to)…………………………………..kusafirisha(To transport)………………………Tani(Tones)…………………….kutoka(From)……………..kwenda (To)……………………………..
2. Kibali hiki ni cha siku (This Permit is valid for number of days)…………kuanzia tarehe ( starting from)………………..mpaka (To)……………………..
3. Kibali hiki hakihamishiki (Not transferable)

KWA MATUMIZI YA OFISI TU (For office use only)
Namba ya kibali (Permit No.) ……………. Tarehe (Date)……………. Mahali (Place)…………….
Stakabadhi Na. (Receipt No.) ………………………ya Tarehe (Date)………………………….

Jina la Afisa Muidhinishaji (Name of Authorizing Officer) ………………………………….
Saini (Signature)……………………cheo (Designation)………………………….

Muhuri (official stamp)

______________

JEDWALI LA PILI

______________

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 16)

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mbarali, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU :
Jina:…………………………………..…………………….....
Saini……………………….…………………………..………
Wadhifa: ………………………………………………………
Tarehe………………………………………………………...

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Mbalali imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Mbalali uliofanyika Tarehe 28 Mwezi 4 Mwaka 2023 na Kushudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

MISSANA K. KWANGURA
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mbalali*

*TAMIMU T. LUBANDAMO*
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Wilaya ya Mbalali*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*